BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

MEI, 2026

BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukwani,Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**Mheshimiwa Spika;** napenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema na neema zake zilizotuwezesha kukutana tena katika Baraza hili Tukufu, tukiwa salama na wenye afya njema. Kukutana kwetu leo ni ishara ya dhamira ya pamoja ya kuendelea kutumikia wananchi na maendeleo ya Taifa letu. Sambamba na hilo, nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha hotuba ya maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu kama Kanuni ya 103(6) kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2024 zinavyoelekeza.

**Mheshimiwa Spika;** kwa unyenyekevu na kwa niaba ya kamati, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa juhudi zake za kuimarisha utawala bora na kuimarisha mazingira ya watumishi wa umma. Tunamuomba Mwenyez Mungu azidi kukulinda na kukupa umri mrefu, wenye imani ya kuendelea kuyajali maisha na maslahi ya wananchi wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika;** vilevile, natoa shukrani zangu za dhati kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Dkt. Mwalim Haroun Ali Suleiman, pamoja na watendaji wote wa Ofisi hiyo, kwa ushirikiano wao wa karibu na wa kujenga waliouonesha kwa Kamati. Ushirikiano huo umeimarisha utendaji na kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya kamati yakiwemo ya upitiaji wa randama ya

Makadirio ya bajeti kupelekea kumalizika bila ya vikwazo.

**Mheshimiwa Spika:** kwa heshima kubwa, na kwa kutambua mchango wao muhimu pamoja na ushauri katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati hii, naomba nichukue fursa hii kuwatambulisha Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa kuwataja majina yao kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Aza Januar Joseph | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Mmanga Mohammed Hamed | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Mahfoudh Abdalla Mohammed | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Masoud Amour Masoud | Mjumbe |
| *7.* | Mhe. Mahmoud Ali Shineni | Mjumbe |
| *8.* | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| *9.* | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu |
| *10.* | Ndg. Shawana Mohammed Haji | Katibu |
| *11.* | Ndg. Hassan Lila Mrisho | Afisa bajeti |
| *12.* | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani |

**Mheshimiwa Spika;** Kanuni ya 101 (3) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2024 inaelekeza kwamba kamati itakuwa na Mamlaka ya kumshauri Waziri na kutoa mapendekezo kutokana na bajeti husika.

**Mheshimiwa Spika;** kwa mantiki hiyo, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi imeridhishwa na utekelezaji wa Bajeti ya Ofis Rais,

Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora pamoja na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2026/2027 baada ya kuipitia, kuijadili na kuipitisha siku ya Ijumaa tarehe 24/04/2026 na hatimae kutoa mapendekezo na sasa kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mapendekezo hayo kama ifuatavyo:

**Mheshimiwa Spika;** Ofisi ya Rais-Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala bora kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 imeelezwa kwamba itatekeleza malengo yake kupitia mafungu ya kibajeti 11 na programu Kuu 14, ambapo Programu 10 zitatekelezwa na Taasisi zinazojitegemea na programu 4 za Fungu 005 zitatekelezwa na Idara zilizo chini ya Katibu Mkuu.

**Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Sheria**

**Mheshimiwa Spika;** Idara ya Katiba na Msaada wa Kisheria ni chombo muhimu katika kuratibu masuala ya katiba na kuhakikisha upatikanaji wa huduma za msaada wa kisheria kwa wananchi, kwa lengo la kusogeza haki karibu zaidi na jamii na kuimarisha utawala wa sheria.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Ofisi ya Rais – Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma kupitia Idara ya Katiba na Msaada wa Kisheria kwa mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya "Mama Samia Legal Aid Campaign", inayotekelezwa kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mafanikio haya yanaakisi dhamira ya Serikali ya kuhakikisha huduma za haki zinawafikia wananchi wote, hususan walioko maeneo ya vijijini.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati inaitaka Idara hiyo kupitia programu ndogo ya **S0201** ya Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Sheria, kusimamia kwa karibu utekelezaji wa awamu ya pili ya Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, ili kuongeza wigo wa huduma, kuimarisha uratibu na kuhakikisha wananchi wengi zaidi wananufaika na huduma hizo muhimu.

**Programu ya Uendelezaji wa Watumishi wa Umma.**

**Mheshimiwa Spika;** wakati wa utekelezaji wa kazi za bajeti, Kamati ilibahatika kukagua mradi wa ujenzi wa Taasisi ya Utawala wa Umma – Pujini, Unaojengwa na Kampuni ya "Modern Building Constractors Ltd" wenye thamani ya shilingi Bilioni Kumi na Tatu, Milioni Mia Tano na Thalathini na Moja, Laki Tatu  Hamsini na Sita Elfu, Mia Tatu na Ishirini (13,531,356,320/=) Mradi huo ulioanza rasmi mwezi Febuari 2026, bado umekuwa ukisuasua kwa madai ya changamoto za mvua, huku ukitarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2026. Kutokana na hali hiyo, Kamati inasikitishwa na kuona kasi ndogo ya utekelezaji wa mradi, jambo linaloashiria udhaifu katika usimamizi wa mradi huo.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati inaitaka Ofisi ya Rais – Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala bora kuchukua hatua za haraka na madhubuti kuhakikisha mkandarasi anaongeza kasi ya ujenzi bila kisingizio cha hali ya hewa, kwa kuzingatia kuwa changamoto za mvua ni jambo linaloweza kutabirika. Aidha, Kamati inaelekeza kuwepo kwa usimamizi wa karibu na wa mara kwa mara ili kuhakikisha mradi unakamilika ndani ya muda uliopangwa na kwa viwango vinavyokubalika. Kamati haitasita kuchukua hatua za ushauri na ufuatiliaji dhidi ya wahusika wote watakaobainika kuchangia ucheleweshaji wa mradi huo.

**Programu ya Usimamizi na Upatikanaji wa Haki - Mahkama Kuu Zanzibar.**

**Mheshimiwa Spika;** katika taasisi za serikali, ukusanyaji mapato ni mchakato wa kukusanya fedha zinazotokana na huduma au adhabu zinazotolewa na taasisi hiyo. Mfano katika Mahakama hukusanya mapato ya serikali kupitia faini zinazotozwa kwa wakosaji pamoja na ada mbalimbali za mahakama (court fees) zinazolipwa na wananchi wanapopata huduma za kisheria. Mapato hayo huwasilishwa kwenye hazina ya serikali kwa matumizi ya umma. Kwa Mwaka 2026/2027, **fungu 026** la Mahakama Kuu Zanzibar imepangiwa kukusanya Mapato ya Serikali kiasi cha shilingi Milioni Mia Nane na Tano, Laki Moja na Sabiini na tatu Elfu (805,173,000) yatokanayo na ada za Mahkama pamoja na faini mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati inashauri Serikali kuwa katika mchakato wa kupanga malengo ya makusanyo ya mapato kwa taasisi za umma, ni muhimu kufanyika tathmini ya kina na ya kiuhalisia kuhusu uwezo wa taasisi husika katika kukusanya mapato. Hatua hiyo, itasaidia kuhakikisha kuwa malengo yanayowekwa yanaendana na uwezo halisi wa utekelezaji, kupunguza changamoto za kushindwa kufikia malengo na kuimarisha usimamizi wa mapato ya Serikali.

**Programu ya Haki na uwezeshaji Kisheriah- Kamisheni ya wakfu na Mali ya Amana.**

**Mheshimiwa Spika;** kupitia Programu Kuu ya Usimamizi wa Haki na Uwezeshaji Kisheria, mojawapo ya malengo ya uendeshaji wa **fungu 054** la Kamisheni ni kuimarisha usimamizi wa mirathi ya Kiislamu, kusimamia mali za wakfu na amana, kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Ibada ya Hija, pamoja na kukusanya na kugawa zaka, sadaka na misaada ya kheri, kama ilivyoainishwa katika Programu Ndogo ya **S0201.**

**Mheshimiwa Spika;** ili kuimarisha utekelezaji wa majukumu hayo, Kamati inaiomba Serikali kwa mwaka huu wa bajeti kuharakisha mapitio ya Sheria ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Nam 2 ya Mwaka 2007, ili kuweka mazingira wezeshi yatakayoiwezesha Kamisheni kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kwa kuzingatia mahitaji halisi ya jamii.

**Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar.**

**Mheshimiwa Mwenyekiti;** Ofisi ya Mufti ni taasisi ya juu ya uongozi wa masuala ya Kiislamu inayosimamia, kuratibu na kutoa miongozo ya kidini kwa Waislamu. Miongoni mwa majukumu ya ofisi hii ni kutoa tafsiri na ushauri wa kisheria za Kiislamu (fatwa), kusimamia masuala ya ibada na maadili ya dini, pamoja na kuimarisha umoja na maadili mema katika jamii ya Kiislamu.

**Mheshimiwa Spika;** kamati inathamini jitihada zinazofanywa na taasisi hii ambazo zinachangia kuongezeka kwa uelewa juu ya masuala ya dini, kiimani na kijamii yanayotokakana na ubora wa majukumu ya ofisi katika utekelezaji wa kazi zake.

**Mheshimiwa Spika;** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Ofisi imepangiwa kutumia jumla ya **Shilingi Bilioni Tatu na Milioni Tisiini na Tatu (3,093,000,000)** kwa ajili ya mishahara na matumizi ya kawaida. Kutokana na ongezeko la majukumu na umuhimu wa huduma zinazotolewa kupitia **fungu la 053**, Kamati inaiomba Serikali kulipitia upya fungu hilo na kuliongezea mgao wa fedha, ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu yatayokidhi mahitaji halisi ya wananchi wanaohudumiwa.

**Programu ya Usimamizi wa Maadili ya Viongozi- Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma**

**Mheshimiwa Spika;** Sote ni mashahidi kwa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma inayofanya kazi za kuhakiki taarifa za rasilimali na madeni ya viongozi wa umma kila mwaka. Kamati inaipongeza Tume kupitia **fungu 113** kwa kazi nzuri inayofanya hususan, kwa kuzingatia uwazi na uaminifu katika kuwasilisha taarifa zake za fedha kila mwaka katika Baraza la Wawakilishi.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati inasisitiza Tume kuifanyia marekebisho Sheria ya Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya Mwaka 2015 kwa lengo la kuimarisha fomu zinazotumika katika uwasilishaji wa taarifa. Imebainika kuwa fomu hizo zina taarifa zinazojirudia mara kwa mara, hali inayosababisha urasimu usio wa lazima. Hivyo, Kamati inaelekeza kuandaliwa kwa mfumo utakaowezesha viongozi kujaza taarifa mpya pekee kwa kila mwaka, ili kurahisisha zoezi hilo na kuboresha ubora wa taarifa zinazowasilishwa.

**Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu Uchumi.**

**Mheshimiwa Spika;** kwa upande wa **fungu 035** la Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi, imekuwa ikitekeleza majukumu yake ya msingi ikiwemo udhibiti wa vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi na ufuatiliaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika;** vile vile, Kamati inatoa pongezi kwa Mamlaka kwa hatua nzuri iliyofikiwa katika mradi wa ujenzi wa jengo lake jipya la makao Makuu na la kisasa

liliopo katika hatua nzuri ya utekelezaji. Aidha, Kamati inasisitiza kwa Mkandarasi kuhakikisha anakamilisha ujenzi wa mradi huo kwa mujibu wa masharti ya mkataba, kwa kuzingatia muda, ubora na viwango vilivyokubalika, ili kuwezesha huduma zinazotolewa na Mamlaka hiyo kuimarika zaidi.

**Hitimisho**

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla Kamati inatambua na kuthamini hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuimarisha ustawi wa watumishi wa umma na kuboresha utendaji wa taasisi zake. Juhudi hizi ni muhimu katika kuhakikisha utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Sambamba na hilo, Kamati inasisitiza umuhimu wa kuendelea kuimarisha usimamizi wa fedha kwa kuhakikisha kuwa bajeti zinazoidhinishwa na Baraza lako Tukufu zinatolewa kwa wakati na kwa ukamilifu wake ili kuwezesha utekelezaji wa mipango ya maendeleo iliyokusudiwa. Kamati inaamini kuwa kwa ushirikiano wa karibu kati ya Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango pamoja na Wizara husika, malengo yaliyowekwa yanaweza kufikiwa kwa tija zaidi na hivyo kuchangia maendeleo ya nchi yetu kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika;** kwa mara nyengine tena napenda kutumia fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha hotuba ya maoni ya Kamati kuhusu Bajeti ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ndani ya Baraza lako Tukufu. Vilevile, nawapongeza Waheshimiwa Wajumbe wote kwa utulivu, umakini na usikivu waliouonesha wakati wa uwasilishaji.

**Mheshimiwa Spika;** baada ya maelezo haya, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe kutoa, maoni na mapendekezo na hatimaye nawaomba waipitishe Bajeti hii baada ya kujadili na kufikia muafaka wa hoja zitakazojitokeza wakati wa mjadala, ili kumuwezesha Mheshimiwa Waziri kutekeleza kikamilifu mipango aliyojipangia katika mwaka wa fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika;** kwa niaba ya Kamati naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na naomba kuwasilisha.

…………….………………..

*(Machano Othman Said)*

Mwenyekiti,

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,

**BARAZA LA WAWAKILISHI,**

**ZANZIBAR**